**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

**Mheshimiwa Spika,**
Awali ya yote, hatuna budi kumshukuru Allah Subuhanahu Wataala kwa kutujaalia uhai pamoja na afya njema, ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kiujumla. Ninamuomba Allah Mtukufu azidi kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, napenda kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako wa Baraza hili, ambao ni Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Allah awazidishie busara na hekma katika jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika Muhimili huu muhimu wa Dola.

Vile vile, pongezi za pekee ziende kwa Uongozi nzima wa Wizara hii kwa juhudi zao kubwa na mashirikiano wanayotuonesha katika utekelezaji wa kazi zetu, Kamati inawata waongeze juhudi katika kutekeleza pamoja na kusimamia majukumu yao kwa ubora na ufanisi zaidi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**,
Kwa kweli, itakuwa si busara iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii kwa namna wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,**
Naomba kuchukua fursa hii kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zawadi Amur Nassor | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| *9.* | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kanuni ya *108(15)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa mapendekezo hayo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika kujadili utekelezaji huo.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa hivyo, baada ya utangulizi huo sasa naomba kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto ambapo jumla ya mapendekezo yalikuwa 7 tuliyaliwasilishwa kwa Wizara na yote tunashukuru yameweza kuyapatia majibu ya kina.

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati, inapenda kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa juhudi zake alizozichukua katika kuhakikisha kwamba Ustawi wa Jamii unaimarika na kuamua kuunda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuigawa iliyokuwa Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati, inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuingizia fedha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya ununuzi wa gari pamoja na ujenzi wa uzio kwa ajili ya Nyumba ya Wazee Limbani Pemba kama walivyopanga kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023, ili wazee waendelee kunufaika na matunda ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, Kamati inasisitiza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuwafanyia uchunguzi wa afya watoto wanaoishi katika Vituo vya Kulelea Watoto kwa kila kipindi kwa lengo la kuweza kuwakinga watoto hao na maradhi tofauti ikiwemo maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza, ili Taifa liwe na nguvu kazi yenye afya njema, kwani Waswahili wanasema "Watoto wa leo ndio Taifa la kesho au nguvu kazi ya kesho".

Pia, Kamati inaiomba Wizara ya Afya kuwapatia daktari Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya Wazee wanaoishi Nyumba ya Wazee Limbani, kwa lengo la kuweza kupatiwa huduma za kimatibabu wakiwa katika nyumba hiyo, ili kuwapunguzia usumbufu wakati wanapohitaji huduma hizo katika hospitali kwa sababu wengine ni watu wazima sana.

## WARATIBU WA SHEHIA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati, inawapongeza Waratibu wa Shehia kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa moyo wa uzalendo na kujitolea licha ya mazingira magumu wanayokabiliana nayo katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku kuhusu kushughulikia masuala ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

**Mheshimiwa Spika,**

Licha ya jitihada hizo wanazozichukua katika kukabiliana na vitendo hivyo, bado Waratibu hao wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa posho ya ufuatiliaji ya kila mwisho wa mwezi ambayo ni shilingi elfu ishirini (20,000/=) kwa kila mwezi, kwa bahati mbaya posho hiyo haipatikani kwa wakati na wakati mwengine kupatiwa kila baada ya miezi mitatu. Hivyo, Kamati inaiomba Wizara kuwaongezea posho la ufuatiliaji kwa Waratibu ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

## VITUO VYA MKONO KWA MKONO

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati, inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Vituo vya Mkono kwa Mkono, yaani One Stop Center kwa ajili ya kutoa huduma kwa wahanga wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji hususan wanawake na watoto katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba na lengo ni muda wa masaa ishirini na nne (24) vituo viwe vinatoa huduma.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa bahati mbaya vingi kati ya vituo hivyo vinatoa huduma chini ya masaa 24 kutokana na changamoto mbali mbali ikiwemo uchache wa wafanyakazi na wataalamu. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiomba Serikali kupitia Taasisi zake zinazohusika na masuala ya kuviendesha Vituo vya Mkono kwa Mkono ikiwemo Jeshi la Polisi, Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhakikisha wanapatikana wataalamu au watendaji kwa ajili ya vituo hivyo, ili viweze kutoa huduma kwa masaa 24 na kuweza kufikia malengo ya uanzishwa wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hayo, Kamati inayapongeza mashirika na taasisi binafsi zinazoshirikiana na Serikali katika kupambana na kupiga vita vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanawake na watoto pamoja na kutoa wito kwa jamii na kuziomba taasisi nyengine kushirikiana

kwa pamoja katika kupambana na tatizo hilo na hatimae liweze kuondoka katika jamii yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa, Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mzuri.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maelezo hayo machache, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

………………………,
Mhe. Mohamed Ahmada Salum,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**